**KENYATTA UNIVERSITY**

**UNIVERSITY EXAMINATIONS 2016/2017**

**SECOND SEMESTER EXAMINATION FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF ARTS**

**AKS 402: KISWAHILI POETRY**

**DATE: TUESDAY 9TH MAY 2017** **TIME: 8.00 A.M. - 10.00 A.M.**

---

**MAAGIZO: JIBU MASWALI MATATU. SWALI LA KWANZA IN LA LAZIMA**

1. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuatia: (Alama 30)

Naomba karatasi, hadithi niwandikie,
Muwe wangu wafuasi,ngano hii iwafikie,
Niwaeleze kiasi,nitakacho mkijue
Hino safari ya chuo,changamoto zake nyingi!

Ni Kaunti umefika, yenye wingi wa mawanda,
Kikosa mbinu hakika, utabaki tu kuwanda,
Tajuta huku kufika,kubaki pweke uwanda,
Hino safari ya chuo, changamoto zake nyingi!

Mazuri mengi mambo,na mengineyo mabaya,
Yanata ovu majambo,mengine yaso mabaya,
Kipima tavuka ng'ambo, la sivyo tavuna haya,
Hino safari ya chuo, changamoto zake nyingi!

La kwanza ni la mavazi,yasokuwa na mipaka,
Yanipayo bumbuazi,msione ni dhihaka,
Mavazi yenye uwazi,ukiona wapofuka,
Hino safari ya chuo,changamoto zake nyingi!

Yapo ya kunata mavazi,megine ya kukatika,
Yaliyo macho mavazi, na ya macho kukatika,
Ya mgongo ulo wazi,tumbo na guu katika,
Hino safari ya chuo,changamoto zake nyingi!

La pili ni mitihani, isokuwa na huruma.
Ikuwekayo taabani,saa zote kuhemahema,
Mitihani iso soni,imejawa na hujuma
Hino safari ya chuo, changamoto zake nyingi!



*INVOLVEMENT IN ANY **EXAMINATION IRREGULARITY** SHALL LEAD TO **DISCONTINUATION***

Yataka ukakamavu,'hadhara kujumuika.
Mengine ni majivu,hepea kujumuika,
Washika na Wazamifu,ukitaka kutajika,
Hino safari ya chuo, changamoto zake nyingi!

La tatu ni wafadhili, wa nipe nami nikupe,
Masiponza wasojali, huwapenda walo kupe,
Chuoni bila akili, utaoza tukuzike,
Hino safari ya chuo, changamoto zake nyingi!

Ridhika chako kidogo, katu sitake bwerere,
Chudi kifanya kidogo,tapata viso vya bure
Hatuazo japo ndogo,zakulisha japo pure,
Hino safari ya chuo,changamoto zake nyingi!

Maadili ni lingine, kilelecha kila kitu,
Yaleta nalo lingine,nidhamu kwa kila mtu,
Jitume bila mwingine,kufanikiwa ki utu,
Hino safari ya chuo, changamoto zake nyingi!

Ya mwisho msilojua, ni kuwa natamatisha,
Ya chuoni nayatua,maana yezatapisha,
Gakuo 'wapa wosia, tahadharini maisha,
Hino safari ya chuo, changamoto zake nyingi!

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama 2)

(b) Lihakiki shairi hili kwa kuzingatia arudhi ya ushairi. (Alama 5)

(c) Mshairi ametaja changamoto kadha zinazokumba wasafiri katika chombo alichokitaja. Taja na ufafanue zozote nne kati yazo. (Alama 4)

(d) Fafanua ushari wa mtunzi kwa wasafiri kuhusu namna ya kuapiku matatizo yanayowakumba. (Alama 4)

(e) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (Alama 4)

(f) Fafanua maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (Alama 4)

- Kuwanda
- Wazamifu
- Masiponza
- Kilelecha


*INVOLVEMENT IN ANY **EXAMINATION IRREGULARITY** SHALL LEAD TO **DISCONTINUATION***

(g) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

(h) Taja na ufafanue kwa kutoa mifano tamathali zozote tatu alizotumia mtunzi. (Alama 3)

2. Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu sawa na historia ya Mswahili mwenyewe. Jadili. (Alama 20)

3. Fafanua mawazo ya Wanajadi yakiopelekea kuibuka kwa mgororo wa ushairi wa Kiswahili. (Alama 20)

4. Fafanua dhamira zozote tano muhimu katika ama; Utenzi wa Al-Inkishafi au, Utezi wa Mwana Kupona. (Alama 20)

5. Jadili sababu za ugumu wa ushairi wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili. (Alama 20)

6. Kwa kurejelea ushairi wa ama; Shaaban Robert, Euphrase Kezilahabi au Kitula King'ei, jadili hoja zozote tano zenye ushairi muhimu kwa jamii ya leo ya Wakenya. (Alama 20)

******************



*INVOLVEMENT IN ANY **EXAMINATION IRREGULARITY** SHALL LEAD TO **DISCONTINUATION***